

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. JENISTA MHAGAMA (MB), KWENYE
ZIARA YA KUTEMBELEA KITUO CHA UTAFITI, UBUNIFU NA UENDELEZAJI
MIFUMO CHA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA) KILICHOPO CHUO
KIKUU CHA DODOMA NDAKI YA CIVE**

TAREHE 10 AUGUST, 2022.

*Mhe. Dkt. Laurean Ndumbaro; Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora,*

*Mhe. Xavier Daudi; Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora,*

*Bw. Priscus Kiwango; Mkurugenzi wa TEHAMA Serikalini Ofisi ya Rais, Menejimenti
ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

Eng. Benedict Ndomba; Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

Wakuu wa Idara na Vitengo vya wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA);

Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

Wanafunzi wa Mafunzo kwa vitendo kutoka vyuo mbalimbali;

Mabibi na Mabwana;

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Awali ya yote, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku hii ya leo.

Pia ninapenda Kumshukuru, *Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Eng. Benedict Ndomba*, kwa mualiko huu pamoja na watumishi Mamlaka kwa maandalizi haya. Niseme tu hii mara yangu ya kwanza kutembelea kituo hiki.

Ndugu washiriki, Serikali kuititia Tangazo Na. 964 la tarehe 6/12/2019 ilitangaza kuwa tarehe 15 Disemba 2019 kuanza kutumika rasmi kwa Sheria ya Serikali Mtandao na Kanuni zake zilizopitishwa mwanzoni mwa mwaka 2020 ambazo zinatumika katika kutekeleza Sheria hii. Sheria hii inaweka msingi wa kisheria wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 na kuanzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) yenye jukumu la kusimamia, kuratibu na kuendeleza utekelezaji wa Serikali Mtandao, pamoja na kusimamia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika taasisi za umma.

Ndugu Washiriki,

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) inatambua nafasi ya TEHAMA katika kufikia malengo ya Taifa na hivyo kusisitiza haja ya ongezeko la matumizi yake katika utendaji wa shughuli za Serikali na utoaji huduma kwa wananchi.

Pamoja na mambo mengine, Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2003 (iliyohuishwa 2016), ilisisitiza juu ya Serikali kutumia fursa zitokanazo na TEHAMA pamoja na matumizi sahihi na yenye tija ya Mifumo ya TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi wa Taasisi unaosaidia kutatua changamoto za kiutendaji, kudhibiti mapato ya Serikali, kujenga na kuboresha uwezo pamoja na kuimarisha mawasiliano mionganini mwa wadau wa Serikali Mtandao.

Ndugu Washiriki, ili kuhakikisha TEHAMA inatoa matokeo tarajiwa kwa Serikali na kwa wananchi kwa ujumla, jitihada mbalimbali zimefanyika katika maeneo ya Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango vya serikali mtandao, ambayo imesaidia katika kusanifu, kutengeneza na kusanikisha Mifumo na Miundombinu ya Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma.

Ndugu Washiriki, ni kweli kuwa, baadhi ya Mifumo ambayo tunajivunia hadi sasa inatokana na shughuli za ubunifu na utafiti zilizofanywa na vijana wetu kutoka katika vyuo vyetu vya ndani kwa weledi na utalaamu mkubwa, kazi ambazo hapo awali ziliwa lazima zifanywe na wataalamu kutoka nje ya nchi. Mfano wa mifumo hii ni Mfumo wa e-Mrejesho, Mfumo wa e-Mikutano, Mfumo wa e-Dodoso na Mfumo wa e-board.

Ndugu Washiriki, Matumizi ya TEHAMA (Digital Transformation) ndiyo muhimili wa mapinduzi ya 4 ya viwanda. Pamoja na matumizi ya TEHAMA, ubunifu ni moja ya nyanja muhimu sana katika kuendeleza na kuharakisha ukuaji wa uchumi wa kidijitali nchini Tanzania. Vyuo vikuu na taasisi kama vile Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), Tume ya TEHAMA, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), na Taasisi za Elimu na Utafiti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zimekuwa zikichukua hatua mbalimbali za uendelezaji wa matumizi ya TEHAMA pamoja na bunifu na atamizi nchini. Kupitia jitihada hizo, Mwaka 2019, Mamlaka ilianzisha kituo hiki ili kuendeleza tafiti za kina, ubunifu na kujengea uwezo vijana wabunifu na wenye vipaji na uwezo kwenye eneo la TEHAMA.

Ndugu Washiriki, Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yanategemea namna ubunifu unavyoanzishwa na kutumiwa. Serikali ilikwishaandaa Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (URT, MSTHE 1996). Lengo kuu la Sera hiyo ni kufikia hatua ya kujitegemea kitekinolojia na kupunguza uagizajia wa bidhaa na teknolojia kutoka nje

ya nchi. Pia Sera inakusudia kuweka utaratibu wa kutambua, kukuza na kuendeleza vipaji maalum na uwezo katika sayansi na teknolojia kwa Watanzania hususan vijana na kinamama ili wanufaikie na utajiri mkubwa wa vipaji vyao kwa maendeleo ya kitaifa.

Ndugu Washiriki, Kwa kutambua umuhimu wa utafiti na ubunifu katika eneo la TEHAMA Serikali kupitia Hati ya Rais ya Mgawanyo wa majukumu katika tangazo la Serikali Na. GN385/2021 imeipa Wizaya ya Elimu, Sayansi na Teknolojia jukumu la uratibu na utekelezaji wa masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Aidha, kupitia hati hiyo, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imepewa jukumu la kufanya tafiti, ubunifu na uendelezaji wa teknolojia katika Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Ndugu Washiriki, Kama inavyofahamika, tupo kwenye Zama za Teknolojia ya Habari (Information Age), ambapo TEHAMA ndio nyenzo muhimu kuwezesha upatikanaji na uwasilishaji wa taarifa kwa kutumia vifaa, mifumo na miundombinu mbalimbali. Hivyo basi, ili kuendelea kupata faida zitokanazo na matumizi ya TEHAMA, jitihada kubwa zimetekelawa katika masuala ya Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao ili kuendana na kasi ya mapinduzi ya TEHAMA na kuiweka katika mazingira mazuri ya kiushindani katika Uchumi wa kidigitali.

Ndugu Washiriki, Wizara kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao inasimamia na kukiboresha Kituo cha Utafiti na Ubunifu cha Serikali Mtandao. Kituo kinafanya tafiti mbalimbali hasa kwenye teknolojia mpya (emerging technologies) kama matumizi ya Blockchain technologies, Machine Learning, Artificial Intelligence na Internet Of Things (IoT) ili na sisi tusibaki nyuma kama Mh. Rais alivyoelekeza. Pia, kupitia utafiti na ubunifu unaofanyika katika kituo hiki, mifumo mbalimbali imetegenezwa inayotatua changamoto zetu badala ya kutegemea mifumo ya nje ya nchi, kama vile mfumo wa

eMikutano (ambao ni Mfano wa Zoom), edodoso (ambao ni Mfano wa Google Survey) na mfumo eMrejesho unaowezesha wananchi kuwasiliana na Serikali yao moja kwa moja kwa kuwasilisha kero, malalamiko, maoni na maulizo. Lengo ni kutumia TEHAMA kumfikia mwananchi na kumfikishia huduma.

Ndugu Washiriki, Vyuo vikuu ndipo mahali pa kufundishia na kubaini vipaji vya vijana wa Kitanzania waonaweza kufanya tafiti na bunifu mbali mbali katika fani ya TEHAMA. Mamlaka ya Serikali Mtandao inatekeleza programu ya kukuza bunifu kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Programu hizi imefanyika kwa misimu Minne mfululizo kuanzia Mwaka 2019 hadi sasa 2022. Mafunzo hutolewa kwa vitendo na wanafunzi wa vyuo vikuu 33 kwa awamu ya kwanza, wanafunzi 35 kwa awamu ya pili, wanafunzi 55 katika awamu ya tatu na sasa imechukua wanafunzi 72 ambao mnashiriki program hii . Inasisitizwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao wamejikita katika ubunifu na utafiti wa mifumo ya kuboresha huduma za serikali kwa wananchi na shughuli za serikali. Serikali Mtandao wanafanikisha azma hii kwa kushirikiana na vyuo vikuu vinavyotoa mafunzo ya TEHAMA. Hivyo basi program hii ni muhimu sana kwa taifa leo.

Ndugu Washiriki, Namalizia kwa kuwakumbusha kwamba utekelezaji wa Serikali Mtandao unahitaji jitihada na utashi wa pamoja wa viongozi, watendaji, wananchi na wadau wengine. Serikali imeweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria na kimkakati ili kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA yanakuwa na tija katika kuwashudumia wananchi na kuwaondolea kero mbalimbali.

Hivyo, niwaombe mtumie siku hizi za mafunzo kwa vitendo vizuri ili hatimaye mtoke na uwezo na ujuzi utakao kuja saidia Serikali kufanya utoaji wa huduma kwa Umma

kupitia TEHAMA uwe bora zaidi, wenyewe ufanisi, na unaokidhi matarajio ya vizazi nya sasa na vijavyo.

“Ili kuijenga serikali imara ya kidijitali, tunatakiwa kuwa na umoja, tujenge mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya pamoja, tuitumie na kuilinda kwa pamoja, kuongeza juhudini kwenye utafiti na ubunifu pamoja na kuandaa mazingira bora ya kuendeleza uwezo na vipaji nya vijana wetu wabunifu”.

Baada ya kusema hayo sasa natamka kwamba program hii ya Nne ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo nya elimu ya juu kwenye kituo cha ubunifu na utafiti cha Mamlaka ya Serikali Mtandao, yamefunguliwa rasmi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA